BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

---

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo, kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena katika Baraza la Kumi kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Serikali na Taasisi zake katika Baraza hili Tukufu. Kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na afya njema ambayo wenzetu wengine amewanyima fursa hii.

**Mheshimiwa Spika,** pia, napenda kutumia fursa hii adhimu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele yako, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na *Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2022/2023* kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2020* zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, niwapongeza na kuwashukuru kwa dhati viongozi wa Ofisi hii wakiongozwa na Waziri wao Mheshimiwa Masoud Ali Mohammed, Katibu Mkuu Ndugu Issa Mahfoudh Haji Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa pamoja Afisa Mdhamini Pemba na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu na kupelekea kutekeleza majukumu yetu

ipasavyo. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makamanda, Maafisa na Wapiganaji wote wa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao waliyotupatia kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, natumia nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia na kutekeleza vyema ushauri na maagizo ya Kamati pamoja na kusimamia kwa ukamilifu na ufanisi utekelezaji wa Bajeti yao ya mwaka *2021/2022*, jambo hili limewawezesha kujenga ari ya kuwasilisha mbele ya Kamati yetu, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio mapya ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha *2022/2023* ili yapate baraka za Wajumbe wako na kwa madhumuni hayo, tunaliomba Baraza lako liridhie na liipitishe Bajeti hii kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika uongozi wake na kuhakikisha maendeleo ya watu na ustawi wa jamii nchini umeimarika pamoja na kusimamia maendeleo ya kiuchumi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984*, kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora unafanikiwa kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati yangu kuwa, mafanikio yanayopatikana katika uimarikaji wa uchumi wetu na huduma za kijamii yanatokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka *2020/2025*.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imekadiriwa kufanya kazi kwa kuzingatia malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na inaakisi hali halisi ya uchumi wetu na harakati za kupunguza umasikini lakini pia kwa kuzingatia malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** pia, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya Wajumbe wa Kamati yangu wakati tulipoipitia bajeti hii, kwa kuonesha umahiri na mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

Naomba sasa niwatambue Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imetumia uweledi wake wa hali ya juu katika kupitia, kuchambua na kujiridhisha vyema na programu zote zilizokusudiwa kufanyiwa kazi kupitia Mafungu ya Bajeti ya Wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2020*.

**Mheshimiwa Spika,** ni imani ya Kamati hii kwamba kupatikana kwa fedha zilizopangwa katika Wizara hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ukamilishaji wamalengo yaliyokusudiwa kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi iliyotengwa katika bajeti hii ya mwaka wa fedha *2022/2023*.

## PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D 01)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya usajili wa wajasiriamali katika Mabaraza yetu na hivyo kushindwa kutoa vitambulisho kwa wajasiriamali hao licha ya kuwepo maagizo ya Serikali kwa muda mrefu. Kamati

inasikitishwa na kuona zipo baadhi ya Halmashauri na Mabaraza ya Manispaa mpaka leo bado wapo chini ya asilimia 10 ya vitambulisho walivyotoa. Kamati haijaridhishwa na suala hili na inaziomba Taasisi husika kuhakikisha wanalifanyia kazi kwa wakati na kwa mujibu wa miongozo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mpango wa kupunguza gharama za malipo ya vitambulisho vya wajasiriamali ambapo kwa sasa wanalipia Tsh. 30,000/- na hivyo, Kamati inapendekeza kupunguzwa kwa kiwango hicho na kuwa Tsh. 20,000/- ili wananchi wengi waweze kumudu gharama hizi kwa wakati.

*Mheshimiwa Spika,* vile vile, Kamati inashauri wakati tunapozipangia Taasisi zetu kukusanya mapato pia, tuzingatie vyanzo vya mapato vya Taasisi husika na uwepo uwiano kati ya Taasisi moja na nyengine. Kwa mfano: kupitia mafungu ya Mikoa wapo waliopangiwa kukusanya kupitia ada ya uhaulishaji Ardhi lakini Mkoa wa Kaskazini Pemba haikupangiwa kukusanya kupitia chanzo hiki ilhali Taasisi zote mbili zinatekeleza majukumu sawa sawa.

*Mheshimiwa Spika,* Katika vipaumbele vya wizara kwa kuzingatia malengo mahususi ya mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi imedhamiria Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweka lengo hili ingawa wasi wasi wetu ni kuona Mamlaka hizi zimeshindwa kutekeleza vyema jukumu la ukusanyaji wa mapato kutokana na upungufu mkubwa wa rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi vya kisasa vya kukusanyia mapato.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati yangu pia, inaitaka Wizara kusimamia kikamilifu na kuhakikisha miundombinu ya Mradi wa Mji Salama imekamilishwa kwa wakati na kukabidhiwa kwa Wizara ukiwa katika hali nzuri na yenye mafanikio kwa nchi yetu ya Zanzibar. Aidha, Kamati inashauri kuongeza wigo kwa maeneo ya Kaskazini Unguja, kaskazini Pemba na Kusini Unguja ili nayo yawe katika Mradi wa Mji salama hasa katika maeneo ya Utalii.

PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D 02 – D 06)

*Mheshimiwa Spika,* Kamati imeridhishwa na kazi nzuri za wapiganaji wetu wa vikosi vya SMZ kwa kushirikiana na vikosi vya SMT kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kuhakikisha kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu, tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kuwapa uwezo askari wetu wa kuitumikia vyema nchi yao.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati yetu inavishukuru na kuvipongeza vikosi vyote vya Idara Maalum za SMZ kwa kutekeleza vyema agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kujiimarisha kwa kuanzisha miradi ya maendeleo ambayo italeta tija kwa vikosi hivi ili kuepuka utegemezi mkubwa wa ruzuku kutoka Serikalini. Aidha, Kamati inashauri vikosi hivi kuhakikisha miradi wanayoanzisha imekuwa na mikato bora na yenye tija na haitaleta athari kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

*Mheshimiwa Spika,* kwa upande mwengine Kamati yangu imebaini kuwepo kwa changamoto ya vitendea kazi vyenye ubora na vinavyoendana na wakati katika shughuli zao za uzalishaji jambo ambalo linapelekea kushindwa kufikia malengo.

*Mheshimiwa Spika*, Kamati inampongeza Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kuviimarisha vikosi vya SMZ na kuimarisha maslahi ya wapiganaji wote wa Idara maalumu. Aidha pongezi za pekee ziende kwa Wakuu wa Vikosi vyote vya SMZ kwa juhudi zao za kusimamia vyema majukumu yao pamoja na kuibua miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika idara zao.

*Mheshimiwa Spika*, katika mipango ya bajeti ya mwaka 2022/2023 kupitia Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Kamati imeridhia mpango wa kuanza kufanyika upembuzi yanikifu na kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa Rada ambazo zitatumika kuimarisha ulinzi wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwani hili ni suala ambalo mara nyingi tumekuwa tukiishauri Serikali kufanya hivyo. Aidha, Kamati inashauri utekelezaji wa mpango huu ufanyike kwa haraka na kwa kuzingatia viwango vya ubora unaotumika kimataifa kwakuwa suala la ulinzi linahitaji vifaa vya kisasa na vyenye kwenda samabamba na mabadiliko ya teknolojia Ulimwenguni.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati pia, inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Kamanda Mkuu wa KMKM kwa kuanzisha na kuimarisha vyema miradi ya kimkakati kama vile ufugaji wa majongoo ya baharini na ununuzi wa boti ya uvuvi miradi ambayo tayari inatekelezwa na kuanza kutoa matunda. Hivyo, mafanikio ya miradi hii itasaidia sana kikosi hiki kupunguza utegemezi wa fedha za matumizi kutoka Serikalini.

*Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar; Kamati yangu inatoa shukrani zake za dhati kwa uongozi wa JKU katika kusaidia na kukuza sekta ya elimu Zanzibar. Kwa muda wa muongo mmoja sasa skuli za JKU zimekua zikifanya vizuri sana na kuwafanya wananchi walio wengi washawishike katika kuwapeleka watoto wao kupatiwa elimu kwenye skuli hizi. Kamati inawaomba JKU kuzidisha nguvu kwa kuajiri walimu wenye uwezo mkubwa pamoja na kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa vijana wanaosoma katika skuli hizi.

*Mheshimiwa Spika,* aidha, Kamati inaishauri Serikali kuzidi kusimamia na kufuatilia vijana wanaoenda JKU kwa ajili kujitolea kwa lengo la kujiimrisha katika uzalishaji lakini pia kutayarishwa kwa ajili ya ajira za Serikali. Kamati haijaridhishwa na kiwango kidogo cha vijana wanaochukuliwa katika kambi zetu kwa nia ya kujitolea kutokana na idadi kubwa vijana wanaomaliza masomo yao kubakia mitaani kutokana na kushindwa kupata nafasi ya kujiunga na mafunzo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha miundombinu ya mabweni na wakufunzi ili kuzidisha uwezo wa kuchukua vijana wengi kutoka na hamasa ambayo imepatikana katika miaka hii ya karibuni.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati yangu ilifanikiwa kutembelea kambi ya mfunzo ya uongozi kwa JKU Dunga na kuona hatua waliofikia katika uimarishaji wa maendeleo ya kambi, ambapo Kamati inasisitiza kukamilishwa kwa miradi iliyoanzishwa kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa. Hata hivyo, Kamati yangu inatoa pongezi kwa ujenzi wa nyumba ya utawala ambayo inajengwa kwa nguvu za askari wanaopatiwa mafunzo katika kambi. Tunaiyomba Serikali kuunga mkono juhudi zao za kuwapatia fedha za kutosha katika bajeti hii ili kukamilisha miradi yao kwa wakati.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati pia, inawataka JKU kupitia Wakala wa Ulinzi ambao ndio chanzo kikuu cha mapato katika kikosi hiki kuhakikisha wametayarisha mikataba ya ulinzi kwa taasisi wanazozifanyia kazi ili kuepusha upotevu wa fedha na kusababisha madeni yasiyo na ulazima kwa kisingizio cha kutokuwepo kwa mikataba baina ya pande hizi mbili. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maaalum za SMZ kufuatilia kwa ukaribu zaidi madeni yote ya Wakala wa Ulinzi na kuhakikisha yanalipwa kama walivyokubaliana.

*Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Kamati yangu pia, inawashukuru na kuwapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya chini ya Kamishna Mkuu kwa kuwalea, kuwatunza na kuwalinda vijana wetu walioko Chuo cha Mafunzo kwa Unguja na Pemba na kuhakikisha wanapotoka wamekua na tabia njema katika jamii.

*Mheshimiwa Spika,* Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa mahabusu wengi katika Magereza yetu na wanaoongezeka siku hadi siku kutokana na vitendo vya uhalifu vinavyofanyika katika jamii. Kamati inaiomba Serikali kuangalia kwa jicho huruma kikosi hiki kwani matumizi yao ya chakula yamekuwa juu zaidi kwa kuwahudumia wanafunzi na mahabusu kwa wakati mmoja.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati imebaini kuwa Sheria Nambari *1* ya mwaka *1980* ya Chuo cha Mafunzo ina mapungufu ambapo kwa sasa haiendani na mahitaji halisi ya utelekezaji wa kikosi hicho licha ya juhudi kubwa kutumika hapo nyuma za kutaka kuifanyia marekebisho lakini bado lengo lake halikufikiwa. Kamati inaagiza Chuo cha Mafunzo wakae na wataalamu wa Sheria na kuipitia upya Sheria hii kwa lengo la kuifanyia maboresho ili kupunguza changamoto za kisheria ambazo zinajitokeza mara kwa mara.

*Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi; Kamati imebaini kuwepo kwa majengo mengi ya Kikosi ambayo hayana ubora pamoja na vitendea kazi vichakavu na vyenye uwezo mdogo katika kukabiliana na majanga ya moto mijini na vijijini.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati inashauri Serikali kufuatilia vituo vyote vya KZU na

kuanzisha mpango wakuvifanyia matengenezo ili viweze kuwa na hadhi inayolingana licha ya kuwepo mpango wa kuvifanyia maboresho vituo hivyo ambapo umeshaanza kwa upande wa Kaskazini Unguja kupitia kituo cha Mahonda. Kamati pia, inashauri kuboreshwa kwa mazingira ya utendaji kazi katika Vituo hivyo.

*Mheshimiwa Spika,* Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokozi katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji na wahudumu ambao ni wasaidizi wakubwa wakati wa kutokea ajali za moto, pia Serikali isimamie kufanyika mapitio Sheria nambari *7* ya mwaka *1999* ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar.

*Mheshimiwa Spika,* katika kujenga mazingira bora ya kazi na kuimarisha ari ya askari wa Kikosi cha Valantia Zanzibar; Kamati yangu imebaini kwamba barabara nyingi zinazoingia katika Kambi za KVZ ni mbovu na si rafiki kwa askari wanaotumia barabara hizi. Kwa mfano barabara ya kuelekea Makao Makuu ya Kikosi cha Valantia – Pemba hairidhishi hata kidogo na haipendezi kabisa kwa Kikosi kama hiki kuwa na barabara yenye muonekano kama huu.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati kwa mara nyengine inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kusimamia kufanyika kwa matengenezo ya barabara hiyo ambayo ni mbovu mno na hasa katika kipindi hiki cha mvua inazifanya shughuli zao kuwa ngumu na hivyo kuchelewa kwa miradi yao. Aidha, Kamati inamuomba Mheshimiwa Waziri katika wizara hii kufanya ziara ya makusudi kuzitembelea kambi zote za KVZ na kuona changamoto zao ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikizungumzwa bila kupatikana utatuzi wake wa pamoja. Sambamba na hilo, Kamati yetu pia inashauri Serikali kukiruhusu kikosi cha KVZ kufanya kazi za Ulinzi wa kibiashara ili kuwa na chanzo cha upatikanaji wa fedha ambacho kitaweza kukidhi mahitaji yao.

## PROGRAM KUUZA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (FUNGU D 07 – D 11)

*Mheshimiwa Spika,* katika programu kuu za Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ujumla wake, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa

Kitaifa imeona utekelezaji wa programu zinazosimamiwa na Tawala za Mikoa pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zaidi katika ukusanyaji wa mapato pamoja na usafi wa miji bado hazijafanikiwa kikamilifu kama malengo yao yanavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na jinsi taratibu za malipo ya wazabuni wa Vikosi vyetu ambao wengi wao ni wazalendo jinsi wanavyocheleweshewa kulipwa fedha zao pamoja na kazi nzuri wanayoifanya. Kamati inashauri Serikali itafute njia sahihi za kuwalipa wazabuni kwa wakati ili kuweza kukamilisha miradi kwa wakati unaokusudiwa.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutafuta utaratibu wa kujenga majengo kwa ajili ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambazo ama majengo yake ni mabovu au hayakidhi mahitaji ili kuwaondolea usumbufu viongozi na watendaji pamoja na wananchi wanaotumia majengo hayo. Aidha, Kamati inaagiza uongozi wa Mkoa wa Kusini Pemba kuhakikisha wanaliendeleza jengo la ofisi ya Mkuu wa Mkoa lililopo maeneo ya Pagali Chake – Chake kwani fedha nyingi zilishatumika katika kulianzisha jengo hili na kama kuna sababu za msingi zilizopelekea kutelekezwa kwa jengo hilo basi ni vyema ikatafutwa sehemu nyengine na ujenzi mwengine ukaanzishwa ili kujenga mazingira bora kwa ofisi hii muhimu katika Mkoa.

*Mheshimiwa Spika,* Katika ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya Maendeleo ambayo inatekelezwa kupitia Mabaraza ya Miji na Manispaa, Kamati yangu inasikitishwa na baadhi ya miradi ambayo inatekelezwa na kusimamiwa na Taasisi hizi kwa kutokuwa na ubora na kushindwa kukamilika kwa wakati. Kamati inazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kutofanya kazi kwa kuridhisha matakwa yao bali wasimamie malengo na shabaha za Serikali katika kuendeleza miradi ya maendeleo.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati inaishauri na kuiomba Serikali kulitazama tena suala la usimamizi wa migogoro ya ardhi pamoja na usimamizi bora wa matumizi yake na kushindwa kuwa na mifumo bora ya matumizi hayo katika utatuzi wa migogoro hiyo inaongezeka badala ya kupungua. Licha ya kuwa *Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari 8 ya mwaka 2014* inawapa uwezo wa kusimamia na kutatua migogoro ya

ardhi, kitu ambacho wahusika kwa masikitiko makubwa wanashindwa kusimamia Sheria hiyo.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati inaishauri Wizara kuongeza juhudi za kuwatengea wafanyabiashara wadogo wadogo maeneo maalum kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao ili kuondoa msongamano wa wafanyabishara ndogo ndogo na wananchi katika maeneo yasiyo rasmi kama vile eneo la Michenzani jumba nambari *7* na *8*, hali inayowaondolea utulivu na faragha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo pamoja na wapita njia.

## WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D 12)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa kuwa na malengo ya kuimarisha huduma za usajili wa matukio ya Kijamii kwa kupunguza muda wa upatikanaji wa hati za usajili wa matukio ya kijamii kwa mujibu wa Sheria. Kamati inaiomba Taasisi hii kuzidisha kasi ya utoaji wa hati hizo kwa jamii ili kupunguza idadi kubwa ya wananchi ambao hawajasajiliwa.

*Mheshimiwa Spika,* Katika kujenga mazingira bora ya kazi na yenye kuleta faraja kwa watendaji wetu ni vyema Serikali yetu tukufu kuangalia kwa kina mahitaji ya Ofisi hii kutokana na changamoto mbali mbali zinazowakwaza katika utendaji wao. Hivyo sasa, Kamati inashauri kutafutwa utaratibu utakaoiwezesha Ofisi hii kuwa na jengo la Ofisi Kuu Pemba ambalo litakidhi mahitaji ya kiofisi kwani ofisi wanayotumia sasa iliyopo Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, haikidhi mahitaji yao na imekuwa ikitumiwa na Taasisi mbili kwa wakati mmoja jambo ambalo si jema chumba kimoja cha ofisi kutumiwa na watendaji wa Taasisi mbili tofauti kwani kufanya hivyo kunarudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii yenye majukumu mazito ya kitaifa.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

*Mheshimiwa Spika,* Kamati yangu inaomba kutoa wito kwa jamii kuhakikisha wanajisajili kila inapobidi kufanya hivyo kwani sheria imebainisha matukio mbali mbali ambayo yanapaswa kusajiliwa ili Serikali iweze kutekeleza vyema mipango yake. Aidha, niwaombe wananchi katika kipindi hiki cha mvua za masika zinazoendelea kunyesha kuzidi kuweka usafi wa mazingira yetu kwa kuepuka kutupa taka kiholela kwenye vyanzo vya maji kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kujikinga na maradhi ya mripuko na malaria ambayo ni hatari kwa nchi yetu.

*Mheshimiwa Spika,* Kamati inaishauri Serikali kupitia mpango mkubwa wa ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maafisa wa Idara Maalumu kuingiza kipengele cha ujenzi wa barabara zinazoingia kwenye vikosi vyote angalau kwa kiwango cha kifusi, kufanya hivyo kutarahisisha kazi zao na kutazisaidia jamii ambazo zinaishi karibu na kambi hizo kwani huzitumia kwa ajili ya kujipatia huduma za kiafya.

*Mheshimiwa Spika,* pia, naomba niwashukuru Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji, uzalendo wao na mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu katika kipindi chote cha maisha ya Kamati hii.

*Mheshimiwa Spika,* kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

*Mheshimiwa Spika,* mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wairidhie, waichangie na waipitishe Bajeti hii na hatimae waidhinishe makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha

*2022/2023* kwa *Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ*.

Mheshimiwa Spika, *Kwa Niaba ya Kamati yangu* Naomba Kuunga Mkono Hoja.

Ahsante,

…………..……………………..

(Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR